

LITANIA YA USHINDI

Ee Mungu Baba kwa namna ya pekee utuvushie mtu huyu kwa salama ili naye atuvushe kutokea sasa na hata baadae ili akiingia kuwa kiongozi wa nchi, basi aiweke misingi ya kiutawala kwa namna ambayo hata akija kiongozi mwingine isiwe tabu kwake kuongoza. Baba ujue tunahitaji taasisi imara na si watu imara. Watu imara wawe ni kwa ajili ya kuongoza na kusimamia taasisi imara na sio mawazo binafsi.

1. Mbeba maono	Tuvushe
2. Mbobezi wa sheria	Tuvushe
3. Mkwepa mauti	Tuvushe
4. Kiboko ya wajuaji	Tuvushe
5. Kipenzi cha wengi	Tuvushe
6. Jabali la hoja	Tuvushe
7. Ngome ya ushindi	Tuvushe
8. Ngao ya haki	Tuvushe
9. Mussa ajaye	Tuvushe
10. Kiongozi jasiri	Tuvushe
11. Mfuasi wa haki	Tuvushe
12. Kimbilio la wanyonge	Tuvushe
13. Kiongozi makini	Tuvushe
14. Chungu cha maarifa	Tuvushe
15. Msaliti wa hujuma	Tuvushe
16. Mfano wa mchungaji	Tuvushe
17. Haiba ya uongozi	Tuvushe
18. Kitanzi cha dhuluma	Tuvushe
19. Shubiri ya wapenda madaraka	Tuvushe
20. Mwanazuoni	Tuvushe
21. Kiama cha mahasidi	Tuvushe
22. Mkweli na muwazi	Tuvushe
23. Heshima ya Taifa	Tuvushe
24. Tunu ya thamani	Tuvushe
25. Amiri Jeshi ajaye	Tuvushe

Ni Yeye hakika. Ni kama wakati uliosubiriwa sana, na ambao unatimia. Tangu mauti hadi uzima, ni nani wa kuizuia mvua isinye juu ya nchi? Ni nani wa kuyazuia maji katika mkondo wake? Hakika haki huinua Taifa. Na wakati uliokubalika ni sasa

NA IWE HIVYO